

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**

SHULE YA SEKONDARI SALAGE,
S.L.P 274,
MASWA.

TAREHE:

Kumb.Na.

MZAZI/MLEZI WA:.....

S.L.P

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020.

1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukuarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kijiunga na Shule ya Sekondari Salage baada ya kuhitimu vizuri Elimu ya Msingi. Ni matumaini yangu kuwa ataitumia nafasi hii ambayo vijana wenzako hawakubahatika kuipata na kulithibitishia Taifa kuwa halikukosea kumchagua. Shule ya Sekondari Salage ni ya kutwa kwa wavulana na wasichana, iliyosajiliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi na kupewa namba ya usajili S.2796

2.0 ENEO NA DIRA YA SHULE.

Shule ya Sekondari Salage iko katika kijiji cha Mwakulilima, Kata ya Nyabubinza, Wilaya ya Maswa umbali wa kilometa 50 kutoka kwenye makao makuu ya wilaya. Dira yake ni kutoa Elimu kwa vijana wote bila ubaguzi wa jinsia, kuandaa vijana wa kitanzania kuwa wachapakazi hodari katika kazi za kuajiriwa na kujajiri.

MAHITAJI YA SHULE.

3.0 SARE YA SHULE.

- Ili kuwepo mfanano wa sare na nidhamu ya uvaaji, mwanafunzi anapaswa kuwa na;-
1. Shati mbili (2) nyeupe za tetroni mikono mifupi zisizobana na zinazochomekwa ndani ya sketi au suruali (wote).
 2. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye kamba (gidamu) za kufungia, visivyo na visigino virefu, urembo, wala visivyo chongoka mbele (wote).
 3. Viatu vya raba na bukta blue bahari wavulana na T- shirt za kijivu wote, wasichana waje na track suti rangi blue bahari kwa ajili ya michezo.
 4. Suruali mbili (2) za rangi Dark blue kitambaa cha suti zenyne marinda, zisizobana, zisizo modo, zisizo na mifuko ya kubandika wala zenyne mfano wa jeans kwa (wavulana).
 5. Mkanda mweusi wa ngozi wa suruali unaoendana na luksi za suruali iliyoshonwa (wavulana) pamoja na Soksi nyeupe jozi mbili (2) wote na tai ya rangi ya dark blue.
 6. Sketi mbili (2) rangi ya Dark blue kitambaa cha suti, zenyne rinda box moja mbele na moja nyuma, zinazofunika miguu kabisa (wasichana).

4.0 VIFAA VYA MWANAFUNZI AWAPO DARASANI.

1. Kamusi (Dictionary) ya kiingereza kwa kiingereza
2. Mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical sets)
3. Mfuko kwa ajili ya kubebea madaftari (School bag) ya kuvalia mgongoni.
4. Madaftari makubwa kumi (10), kalamu ya wino, penseli, kifutio na rula.

5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kujifunza kwa makini darasani na kurudi saa 10 jioni (preparation) ni lazima kwa kila mwanafunzi.
- (d) Kuwahi asubuhi na kushiriki katika shughuli zote za shule utakazopangiwa na walimu.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaal sare ya shule wakati wote uwepo shulenii na mahali unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (i) Kutunza mali za Umma.

6.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- (a) Wizi.
- (b) Uasherati na ushoga.
- (c) Ubakaji.
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- (e) Kupigana/kupiga.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kutoa mimba.
- (i) Kuoa au kuolewa.
- (j) Kugoma, kuchochaea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- (k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- (l) Kuwa na simu ya mkononi.

MUHIMU.

Kila mwanafunzi anatakiwa kutii sheria, kanuni na taratibu zote za shule kwa kadri zitakavyotolewa. Kuzikiuka sheria, mwanafunzi hatavumiliwa na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

Unatakiwa kuripoti tarehe 11/01/2020 siku hiyo mwanafunzi afike shulenii akiwa na mahitaji yote yanayotakiwa akiambatana na mzazi/mlezi wake, bila hivyo hatapokelewa. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2020.

NB: Kabla ya kuja shule, hakikisha fomu A na B zilizoambatanishwa pamoja na barua hii zimejazwa kikamilifu na kusainiwa na wahusika.

Nakukaribisha sana katika Shule ya Sekondari Salage.

Wako,

.....
EMMANUEL E. LUSWAGA
MKUU WA SHULE.
Mawasiliano: 0787 - 931847

*HEADMASTER
SALAGE SECONDARY SCHOOL
FEBRUARY 2024
MAGY*

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUFUATA
SHERIA ZA SHULE.**

1. Jina la Mwanafunzi
2. Tarehe ya kuzaliwa:
3. Shule ya Msingi: Namba ya Mtihani
Kata ya Tarafa
4. Jina kamili la baba: Hai / amefariki
Kijiji Kata Tarafa
5. Jina kamili la Mama: Hai / amefariki
Kijiji kata Tarafa
6. Jina kamili la mlezi (kama hana mzazi)
7. Uhusiano na mlezi
8. Kazi ya Baba / Mlezi
9. Jamaa katika familia:-
 - (a) Jina la ndugu wa karibu
 - (b) Jina la ndugu wa karibu
 - (c) Yeye ni wa ngápi katika familia

NB: Nathibitisha kuwa nimesoma na kuelewa vizuri sheria za shule hii na kwamba nathibitisha kuwa sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Ee Mungu nisaidie.

.....
Sahihi ya Mwanafunzi.

FORM B

MASWA DISTRICT COUNCIL

SALAGE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 274,
MASWA – SIMIYU.

DATE:

TO THE MEDICAL OFFICER,

.....
.....
.....

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine the below mentioned girl/boy as to her/his fitness for studies in this school.

(This form must be completed by a government medical officer)

Student's full name: _____

Present age: _____

Blood Test: _____

Stool Examination: _____

T.S. Test: _____

Asthma: _____

Eye Disorder: _____

Skin Diseases: _____

Anemia: _____

Chest: _____

Pregnancy test for girls: _____

Operations: _____

Serious accidents: _____

Physical defects or impairment: _____

Any other infections/Diseases: _____

I certify that I have personally examined Mr/Miss _____ and found
his/he fit to pursue further studies.

Signature _____ Designation _____

Official stamp: _____